

# Tamko dhidi ya Ukeketaji wa Wanawake

2016



HM Government

Ukeketaji (FGM) ni unyanyasaji wa watoto na pia ni zoezi lenye madhara mabaya sana yanayoteketeza afya za wasichana na wanawake. Wasichana wengine hufariki kutokana na kupoteza damu au kuathirika kutokana na utaratibu huu. Wanawake wengine ambao wamekeketwa huweza kupata tabu wakati wa uzazi na huweza kuteseka kwa magonjwa ya akili yanayoendelea kwa muda mrefu.

**Hili tamko lina lengo gani:** Uchukue tamko hili unapoenda safari nje ya nchi. Unaweza kuonyesha familia yako. Hii inaonyesha wazi kwamba kukeketwa ni **kosa kubwa la jinai** Uingereza lenye kuweza kumfanya mwenye hatia afungwe jela kwa muda wa miaka isiyozidi 14. Wazazi wako, au mtu ye yeyote anayekulea, anaweza kuwa na hatia ya kosa kama atashindwa kukukinga kutokana na ukeketaji.

**Weka tamko hili salama:** Beba tamko hili wakati wote – hasa utakapokuwa nje ya nchi.

**Ukeketaji ni nini:** Ukeketaji ni kukatwa kwa sehemu za siri za mwanamke bila ya kuwepo kwa sababu za kimatibabu. Wakati mwingine hujulikana kama kutahiriwa kwa wanawake au ‘suna’.

**Sheria ya Uingereza:** Ukeketaji ni kosa la jinai Uingereza<sup>1</sup>.

- Hata kama mtu atachukuliwa nje ya nchi ili akeketwe, bado hilo ni kosa la jinai Uingereza kama kukatwa kutafanywa na mtu mwenye uraia wa Uingereza au mkazi wa Uingereza.
- Pia ni kosa la jinai kama mtu mwenye uraia wa Uingereza au mkazi wa Uingereza akimsaidia mtu ambaye hana uraia wa Uingereza au ambaye si mkazi wa Uingereza ili akekete mtu ambaye ni raia wa Uingereza au mkazi wa Uingereza wakiwa nje ya nchi.

---

1 Uingereza, Uwelsi na Ireland ya Kaskazini, utaratibu huu ni uvunjaji wa sheria chini ya sheria ya Ukeketaji ya mwaka 2003. Nchini Scotland ni uvunjaji wa sheria chini ya sheria ya kupiga marafuku ukeketaji ya mwaka 2005.

- Na kama kukeketwa kukifanywa kwa msichana ambaye ana umri wa chini ya miaka 16, basi kila mtu anayehusika na kumlea msichana huyo wakati huo atakuwa na hatia<sup>2</sup>.

**Adhabu za hatia:** Yeyote atakayekutwa na hatia ya ukeketaji - au hatia ya kumsaidia mtu ili akekete – atawezza kufungwa jela kwa kipindi kisichozidi miaka 14, atapewa faini, au yote mawili.

Yeyote atakayekutwa na kosa la kushindwa kumkinga msichana kutokana na hatari za ukeketaji atawezza kufungwa jela kwa muda usiozidi miaka 7, atapewa faini, au yote mawili.

---

2 Uingereza, Uwelsi na Ireland ya Kaskazini.

**Msaada:** Kama una wasiwasi kwamba jambo hili linaweza kukutokea wewe, au mtu unayemjua, unaweza kuongea kwa siri na mwalimu, daktari, muuguzi wa shule, mfanyakazi wa jamii, afisa polisi au weledi ye yote anayehusika na afya, elimu au msaada wa jamii. Wataweza kukusaidia na kukulinda. Kama wewe ni mwathiriwa wa kukeketwa na utaripoti polisi, basi polisi itaficha jambo hili ili isijulikane kama umeripoti, na hili linatendeka kuanzia pale utakapopeleka madai yako. Hii ina maana kwamba hakuna habari yoyote itakayochapishwa ambayo inaweza kufanya utambulike kuwa ni mwathiriwa wa ukeketaji, hii ni hata kama jambo hili halitopelekwa mahakamani.

Kama upo Uingereza na una wasiwasi kwamba utachukuliwa nje ya nchi kwa kusudi la kukeketwa **tafadhalii piga simu polisi kwa kubonyeza namba 999** .

Kama upo nje ya nchi na unahitaji msaada au ushauri tafadhalii piga simu **Foreign and Commonwealth Office (Ofisi ya Mambo ya Nje)** nambari ya simu  
**+44 (0) 20 7008 1500**

Unaweza pia kupata msaada kutoka:

**NSPCC FGM Namba ya msaada:**  
0800 028 3550  
**Barua pepe:** [fgmhelp@nspcc.org.uk](mailto:fgmhelp@nspcc.org.uk)

**Childline (namba ya watoto)**

Namba ya simu: 0800 1111

**[www.childline.org](http://www.childline.org)**

**Equality Now**

**(mjini Nairobi, Kenya na London, UK)**

Namba ya Simu (London):

+44(0) 20-7304 6902

Namba ya Simu (Nairobi):

+254 20-271-9832

**[www.equalitynow.org](http://www.equalitynow.org)**

© Crown copyright 2016  
(haki zote zimehifadhiwa)

Swahili – 2905975



When you have finished with  
this publication please recycle it